

Deni

Karatasi la uhakika wa muongozo wa pesa zako

Deni ni nini?

Deni hutendeka wakati unapopata kukopa pesa au kupata bili ambazo haujalipia.

Nitapata vipi deni?

Wakati unapokopa pesa kutoka mkopeshaji (mtoaaji mkopo) wewe una deni. Pesa hizi lazima zilipwe na gharama zaidi kama vile faida.

Pia deni yaweza kuwa ya huduma ambayo bado hajailipia. Hii yaweza kuwa bili ya umeme, bili ya simu ya mkono, au bili ya tuvuti.

Ukiwa na shida ya kulipa deni lako, unaweza kufanya mojawapo ya haya:

- ▶ endelea kulipa kiasi chochote unachoweza
- ▶ wasiliana na wale unaowadai na kuwajulisha kuwa unazo shida za kulipa deni lako
- ▶ wasilina na Mshauri wa Fedha bila malipo ili uweze kupata msaada kupangia deni lako.

Kumbuka

- ▶ Deni ni pesa unazodaiwa na unahitaji kuzilipa.
- ▶ Wewe unaweza kuwa na shida za kisheria kama huwezi kulipa deni yako.
- ▶ Kama huwezi kulipa deni lako kwa muda uliyokubalriwa, unaweza kutozwa faida zaidi.

Wapi kupata usaidizi na maelezo zaidi

Kama unazoshida za pesa, wasiliana na Mshauri wa Kifedha bila malipo kwenye simu 1800 007 007.

Kwa maelezo zaidi kuhusu Washauri wa Kifedha na muongozo wa deni lako, tembelea tuvuti ya MoneySmart, www.moneysmart.gov.au, au pigia simu 1300 300 630.



Lewis alipia deni lake lote la kadi ya mkopo

Lewis amefanya kuanzisha biashara ndogo ya kuuza michoro ya rangi katika soko la mtaani. Ili kuanza yeye anahitaji kununua rangi, burashi za kupakia rangi na vitu vingine.

Lewis pia hana akiba na hutumia kadi ya mkopo kununua kila kitu. Yeye hukopa \$1,200 kwenye kadi yake ya mkopo. Lewis anafikiria kuwa akiuza michoro yake ya rangi ataweza kulipia deni ambalo anadaiwa kwenye kadi ya mkopo na kupata pesa zaidi.

Katika soko Lewis aliuza michoro michache tu na akapata \$720 pekee. Lewis alijuwa kuwa hizi pesa hazitoshi kulipia deni la kadi la mkopo. Yeye pia alihitaji pesa zingine alizopata kwenye soko la mtaa ili kununua rangi zingine zaidi. Lewis hakujua lakufanya.

Baadaye usiku huo rafikiye Lewis, Reon alikuja pale. Reon aliuliza Lewis jinsi soko ilivyokuwa. Lewis alimuelezea kuwa yeye hakupata pesa za kutosha ili kulipia pesa zote alizodaiwa kwenye kadi ya mkopo.

Reon alimwaambia Lewis kuwa njia mzuri ya kuongoza deni lake ni kuwa na bajeti. Reon alisema kuwa hii itamsaidia Lewis kujua kiasi gani cha deni ambacho yeye anacho na kiasi gani ambacho anaweza kukulipia. Halafu Lewis ataweza kujua itamchukua muda gani kulipia deni lake.

Reon aliandika mapato ya Lewis kutoka soko. Halafu Reon aliandika vitu vyote ambazo Lewis alihitajika kulipia ikiweco rangi, burashi ya rangi, kodi katika soko pamoja na malipo yake ya kila mwezi kwenye kadi yake ya mkopo.

Sasa Lewis anajihisi kuwa ana utawala. Yeye alijua kiasi gani ambacho ataweza kulipa pole pole kila mwezi kwenye kadi yake ya mkopo. Lewis alifanya kujua kuwa ndani ya miezi mitatu yeye hatakuwa na deni lolote.

This page has been intentionally left blank.